



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA  
OFISI YA RAIS  
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA  
HALMASHAURI YA MANISPAA YA SINGIDA



23/06/2023

TANGAZO LA ZABUNI

ZABUNI YA KUTOA HUDUMA YA KUTENGENEZA WASIFU WA  
UWEKEZAJI MANISPAA YA SINGIDA  
ZABUNI NA. LGA/115/HQ/ 2022/2023/NCS/10

Halmashauri ya Manispaa ya Singida inakusudia kuandaa Wasifu wa uwekezaji kwa ajili ya kutangaza maeneo ya uwekezaji katika Manispaa ya Singida.

Halmashauri ya Manispaa ya Singida inapenda kuwaalika Makampuni, Mashirika, Taasisi, wataalamu binafsi wenye nia na uwezo wa kufanya kazi hiyo kutuma maombi yao.

Zabuni zitaendeshwa kwa mujibu wa sheria ya manunuzi Na.7 ya mwaka 2011 na kanuni zake za mwaka 2013, Tangazo la Serikali No.446 pamoja na marekebisho yake

MASHARTI YA MAOMBI YA ZABUNI

**Maombi yote ya Zabuni yazingatie masharti yafuatayo: -**

1. Nyaraka za zabuni zitapatikana katika ofisi ya Manunuzi No 12 Manispaa ya Singida
2. Ombi la zabuni liwe na Jina na anuani ya mwombaji, aidha aonyeshe mahali ofisi yake ilipo.
3. **ZINGATIO:** Fomu ya maombi ya zabuni ijazwe kikamilifu na kusainiwa na mwenye uhalali wa kisheria (Power of Attorney) katika zabuni hii.
4. Mwombaji atatakiwa aambatanishe kivuli cha TIN Namba
5. Kama Mwombaji ni Kampuni awasilishe kivuli cha usajili wa kampuni, usajili wa VAT/TIN, Tax Clearance certificate iliyo hai vilivyothibitishwa na Wakili na "Power of Attorney", pia ambatanishe vielelezo halali vya kuonyesha umiliki wa kampuni hiyo (memorandum na articles of association/ extract).

6. Mwombaji asiwe na mgogoro au deni lolote analodaiwa na Halmashauri ya Manispaa ya Singida
7. Mwombaji aonyeshe uzoefu wa kazi alionao kwanye zabuni anayoomba usiopungua mwaka mmoja yenye ukubwa wa kazi sawa na zabuni anayoomba pamoja na thamani inaolingana na zabuni aliyoomba akiambatanisha vielelezo vya uthibitisho wa kazi alizowahi kufanya.
8. Mwombaji yeyote atakayeshindwa masharti ya zabuni atakuwa amejiondoa mwenyewe katika ushindani.
9. Mzabuni yoyote atakayotoa taarifa za uongo au nyaraka ambazo sio sahihi kwa ajili ya kupata zabuni hii, pindi itakapobainika zabuni yake itafutwa.
10. Zabuni zitaendeshwa kwa mujibu wa sheria ya manunuzi No.7(2011) na kanuni zake za mwaka 2013, Tangazo la Serikali No.446 na marekebisho yake ya mwaka 2016
11. Zabuni zote zitumwe zikionesha aina ya zabuni, namba ya zabuni. Zabuni zitumwe katika kwa Mkurugenzi kwa anuani ifuatayo: -  
**Mkurugenzi wa Halmashauri,  
Halmashauri ya Manispaa ya Singida,  
S.L.P. 236  
Singida.**
12. Mwisho wa kupokea maombi hayo ni tarehe 05<sup>th</sup> July, 2023 saa 4.00 Asubuhi [saa za Afrika Mashariki].

*Upendo Naftari*  
Upendo Naftari

**KAIMU MKURUGENZI WA MANISPAA  
SINGIDA  
MKURUGENZI WA MANISPAA  
SINGIDA**

Halmashauri ya Manispaa: Karume Road: S.L.P 236, Singida; Simu Na: +255 26 250 2179/2362;  
Nukushi Na: +255 26 250 2179; Barua pepe: [md.singidamc@singida.go.tz](mailto:md.singidamc@singida.go.tz); Tovuti: [www.singidamc.go.tz](http://www.singidamc.go.tz)